



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA KILIMO  
TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA  
TANZANIA



**TAARIFA KWA UMMA**

**SACCOS 691 ZAPEWA LESENI KWA MUJIBU WA SHERIA NA KANUNI ZA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA**

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022, imetoa Leseni kwa SACCOS 691 zilizokidhi sifa na vigezo vya kupewa Leseni kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha na SACCOS moja (1) imefutiwa Leseni yake kutokana na kukiuka matakwa ya Sheria. Orodha ya SACCOS zilizopewa leseni na kufutiwa, inapatikana kwenye Jedwali lililoambatishwa kwenye taarifa hii.

Aidha, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania inaendelea kuutahadharisha Umma kutoendelea kufanya kazi na SACCOS ambazo hazina Leseni nchini. SACCOS zote ambazo hazijaomba na kupata Leseni zinaelekezwa kutoendelea kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha pasipokuwa na Leseni husika. Kuendelea kufanya biashara hiyo ni kwenda kinyume na matakwa ya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na.10 ya Mwaka 2018, Kifungu cha 16(2).

TCDC inazielekeza SACCOS zote nchini kuendelea kutekeleza vyema matakwa ya Sheria na Kanuni zake kama zinavyoelekeza ili kuepuka adhabu na hatua zinazoweza kuchukuliwa kwa kukiuka matakwa ya Sheria zilizopo.

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania inaendelea kutekeleza matakwa ya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na.10 ya Mwaka 2018 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2019 kama mamlaka kasimishwa. Kwa mujibu wa Kifungu cha 16(1) cha Sheria hiyo, SACCOS inatakiwa kuomba Leseni kabla ya kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha nchini. Maombi ya Leseni za SACCOS yanapaswa kuwasilishwa TCDC (kwa njia ya mtandao (<https://www.ushirika.go.tz/index.php/> - sehemu iliyoandikwa *Maombi ya Leseni*) na mara baada ya kupokea maombi hayo, TCDC inafanya uchambuzi na tathmini na kutoa Leseni kwa SACCOS zinazokidhi sifa na vigezo vilivyoelekezwa kwenye Sheria na Kanuni zake.

Tangazo limetolewa na;

**MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA**

8 Julai, 2022